# MAFUNZO YA MAADILI NA UADILIFU KWA VIONGOZI WA UMMA

## MUHTASARI

Kwa kuzingatia misingi ya Maadili iliyoainishwa katika Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398, ambayo yanamtaka kila kiongozi wa Umma kuzingatia viwango vya juu vya maadili ili kukuza utu, uwazi, uadilifu, uwajibikaji na kuimarisha imani ya wananchi kuhusu utendaji wa viongozi wa umma; Ofisi ya Rais, Sekretariet ya Maadili ya Viongozi wa Umma (ES) kwa kushirikiana na Chuo Cha Uhasibu Arusha (IAA) wameingia makubaliano (MoU) ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na ushauri kwenye masuala yanayohusu Maadili ya Viongozi wa Umma. ES na IAA watatoa mafunzo kwa Viongozi wa Umma waliotajwa kwenye kifungu cha 4 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Na.13 ya mwaka 1995, sura 398, kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia tangazo la Serikali na. 857 la tarehe 24/11/2023.

## MALENGO MAHUSUSI YA MAFUNZO

Mafunzo haya kwa viongozi wa umma yana malengo mahususi yafuatayo:

- Kukuza uadilifu na Uwajibikaji, uaminifu na utawala bora miongoni mwa viongozi wa umma.
- Kuongeza uelewa na umuhimu wa misingi mikuu ya maadili katika utumishi wa umma.
- Kuimarisha uwezo wa kufanya maamuzi yenye kuzingatia maadili katika mazingira mbalimbali ya kazi.
- Kuzuia na kupambana na rushwa na ufisadi na kuzipitia kwa kina athari za rushwa na ufisadi kwa maendeleo na usalama wa taifa.
- Kukuza uwazi na uhusiano bora wa viongozi na wananchi wanaowahudumia.
- Kujenga utamaduni wa maadili kwa kuhimiza wafanyakazi wa kila taasisi kuzingatia maadili katika kazi zao.
- Kuongeza Imani ya wananchi kwa serikali yao kwa viongozi kutimiza wajibu wao kwa uadilifu, uzalendo na kuzingatia maslahi mapana ya umma.

## RATIBA YA MAFUNZO

Kiongozi wa Umma aliyetajwa katika ratiba hii, anaombwa kuchagua tarehe na mahali kulingana na nafasi yake kama ilivyooneshwa kwenye ratiba. Ni muhimu kuhakikisha kuwa kila kiongozi anashiriki mafunzo haya ndani ya muda uliopangwa. Baada ya mafunzo kwa makundi haya kukamilika, mafunzo mengine yatakayofuata, yatawahusu viongozi mbalimbali wa umma waliosalia. Aidha, ratiba yao itatolewa pia.

## ADA YA MAFUNZO

Mafunzo haya yatatolewa katika vituo mbalimbali vilivyoainishwa kwenye Ratiba iliyoambatishwa hapo chini (uk.3). Kila mshiriki atachangia **Tshs 1,500,000 kwa kada ya Wakuu wa Idara na Vitengo na Tshs 2,000,000 kwa kada zilizosalia** kwa ajili ya ada ya ushiriki, chai na chakula cha mchana kwa muda wa siku tatu, pamoja na gharama za vyeti, na vitendeakazi mbalimbali vitakavyotolewa wakati na baada ya mafunzo. Malipo yote yafanyike kupitia control number itakayotolewa.

---

## MUHIMU:

Tunaomba majina rasmi ya viongozi kama yalivyo kwenye taarifa za serikali kwa ajili ya vyeti maalum vya kutambua ushiriki wao katika programu nzima ya kukuza maadili nchini.

a. **Tuma majina matatu ya Kiongozi;**
b. **Cheo/Wadhifa wa Kiongozi;**
c. **Barua pepe ya mshiriki na ya taasisi anayotoka;**
d. **Anwani ya Posta ya taasisi;**

➡ **Taarifa hizi zote zitumwe kwenda barua pepe(mojawapo);**

- ec@maadili.go.tz
- bcu@iaa.ac.tz

---

➡ **Unaweza pia kupiga simu zifuatazo:**

- 0752 883 222 | Pamela Evelyne
- 0762901348 | Birigitha John
- 0784 652 823 | Gerald Mwaitebele
- 0687 638 295 | Aneth Mushi

Unaweza pia kutembelea tovuti yetu na kujaza taarifa zako “online” https://bcu.iaa.ac.tz/ chagua kozi inayoitwa “Mafunzo ya Maadili na Udilifu kwa Viongozi wa Umma...” Kisha jaza fomu taarifa zako kikamilifu na bofya “Apply”

# RATIBA YA MAFUNZO KWA VIONGOZI MBALIMBALI WA UMMA

| SN | TAREHE | MAHALI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Machi 17 - 19, 2026 | MWANZA | • Wakurugenzi wa Jiji, Manispaa na Miji<br>• Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya<br>• Mameya wa Jiji, Manispaa na Miji<br>• Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya<br>• Wenyeviti wa Kamati za Madiwani za Majiji, Manispaa, Wilaya na Miji |
| 2 | Machi 25 - 27, 2026 | MOROGORO | |
| 3 | Aprili 15 - 17, 2026 | MOROGORO | • Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma (DAHRMs) |
| 4 | Aprili 22 -24, 2026 | MOROGORO | • Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma |
| 5 | Mei 6 – 8, 2026 | ARUSHA | • Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma |
| 6 | Mei 20 – 22, 2026 | MOROGORO | • Wajumbe wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma |
| 7 | Juni 3 – 5, 2026 | MWANZA | • Wajumbe wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma |
| 8 | Juni 10 – 12, 2026 | ARUSHA | • Wakuu wa Idara na Vitengo katika Wizara, Idara ya Serikali,Taasisi za Umma, Mamlaka za Serikali na Mashirika ya Umma |
| 9 | Juni 24 – 26, 2026 | MWANZA | • Wakuu wa Idara na Vitengo katika Wizara, Idara ya Serikali,Taasisi za Umma, Mamlaka za Serikali na Mashirika ya Umma |

OFISI YA RAIS,
SEKRETARIETI YA MAADILI
YA VIONGOZI WA UMMA

INSTITUTE OF
ACCOUNTANCY
ARUSHA